



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ



MARKAZIL IMAAMIL MUZANIY DAR – ES – SALAAM - TANZANIA

FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUGA NA MARKAZIL IMAAMIL MUZANIY

SIFA ZA KUJIUGA NA MARKAZ

Mwanafunzi atakaejiuga na markazi, anatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

1. Awe mwanamume.
2. Awe ni mhitimu wa shule ya msingi, bila ya kua na sifa ya kuendelea na elimu ya juu.
3. Kwa mwanafunzi wa bweni, umri wake usizidi miaka ishirini na tano(25).

MASHARTI YA MWANAFUNZI ALIESAJILIWA NA MARKAZI

- 1) Mwanafunzi anatakiwa kushiriki vipindi vyote vya masomo.
- 2) kuhudhuria swala zote za faradhi.
- 3) kuhudhuria katika muda wa kujisomea(muraajãa).
- 4) Hairuhusiwi kutoka nje ya Markazi bila ruhusa kutoka kwa wahusika.
- 5) Kutofanya jambo lolote ambalo lipo kinyume na sheria ya kiislaam.
- 6) Ni wajibu kutekeleze kila jambo litakalo elekezwa na uongozi wa markazi.
- 7) Si ruhusa kwa mwanafunzi kumiliki simu ya aina yeyote ile.
- 8) Hairuhusiwi kulala bwenini wakati wa masomo hata kama ni mgonjwa.

KWA
MWAKA
MPYA
WA
MASOMO
2025 - 2026

MALENGO YA MARKAZI

Lengo la markazi ni kutoa elimu sahihi ambayo itamuwezesha mwanafunzi kuwa katika manhaji au njia sahihi inayofuata Qur-ani na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia.

MAHITAJI YA MWANAFUNZI ATAKAPORIPOTI MARKAZI

- 1) Godoro **Jipya** lenye ukubwa wa futi mbili na nusu, pesa ya foronya ya godoro shilingi (15,000), sanduku la bati (TRANKA) na kufuri.lake.
- 2) Mashuka mawili pamoja na chandarua (Net) ya futi mbili na nusu.
- 3) Nguo za kuvaa, kanzu sita, nne za rangi na mbili nyeupe, Shati au t-shirt mbili, Suruari tatu, kofia pamoja na kilemba cheupe na viatu vya kuvaa akiwa ndani ya markazi.(kama yeboyobo).

HAIRUHUSIWI KUZIDISHA IDADI YA VITU ULIOPANGIWA HAPO JUU

- 4) Pesa taslimu bila mapungufu tena kwa awamu moja tu, **(Tsh.370,000/=)** laki tatu na elfu themanini, ndani ya mwaka atakaojiunga na masomo, kwa mwanafunzi wa bweni tu, ama wa kutwa atalipia **(Tsh.80,000)** , ndani ya mwaka atakaojiunga na masomo.
- 5) Aje na pesa yake ya matumizi madogomadogo, vyombo vya kulia, sahani, kikombe, bakuli na kijiko ila visiwe vya plastiki, bila kusahau mswaki, dawa ya meno pamoja na sabuni na ndoo ya lita kumi.

MAHITAJI YA KIOFISI KWA BWENI NA KUTWA

6 Passport size nne(4),pesa ya pakiti moja ya karatasi za kopi (shilingi 12,500), pesa ya usafi na ukarabati mbalimbali shilingi 30,000 barua ya serikali za mtaa yenye picha yake, cheti cha kuzaliwa / kitambuishi cha ulaiya / cheti cha kuhitimu shule na vitambulisho vya mdhamini au mlezi wa mwanafunzi .

VYETI VYOTE NA VITAMBULISHO VIWE NI VYA ASILI (ORIGINOL) SIO KOPI.

MASOMO YANAYOFUNDISHWA MARKAZI

- | | |
|--|-------------------------|
| 1) QUR-AN TUKUFU (KUSOMA NA KUHFADHI) | 11) KANUNI ZA UWANDISHI |
| 2) AQIIDA (TAUHIID) (KUSOMA NA KUHFADHI) | 12) BALAGHA. |
| 3) HADITHI (KUSOMA NA KUHFADHI) | 13) MANHAJ SALAFI |
| 4) FIQHI | 14) USUULU TAFSIIRI |
| 5) HISTORIA YA MTUME SWALA NA SALAAMU ZIWE JUU YAKE. | 15) USUULU FIQHI. |
| 6) TAJWIID (KUSOMA NA KUHFADHI) | 16) KHATWI NA IMLA |
| 7) NAHAU (KUSOMA NA KUHFADHI) | 17) MTWALAA |
| 8) LUGHA YA KIARABU | 18) UBORA WA MASWAHABA |
| 9) KUJIFUNZA KUSOMA NA KUANDIKA | 19) SWARFU |
| 10) TAFSIRI YA QUR-AN TUKUFU | 20) MUSTWALAHUL HADIITH |
| | 21) FARAAIDHU , N.K. |

ZINGATIA HATUA ZIFUATAZO

1. TOA TAARIFA MAPEMA KUPITIA NAMBA HIZI : **0745 228 752 / 0688 745 131 / 0688 139 402**
2. NJOO UKIWA UMETEKELEZA MAAGIZO YOTE BILA MAPUNGUFU TENA KWA WAKATI SAHIHI.
3. TAREHE YA KUPOKEA WANAFUNZI NI: **13/04/2025** , SIKU YA JUMAPILI.
4. UKICHELEWA KURIPOTI, HUTOPOKELEWA.
5. MUDA SAHIHI WA KURIPOTI NI KUENZIA SAA KUMI NA MBILI ASUBUHI MPAKA SAA SITA NA NUSU MCHANA.
6. GHARAMA YA FOMU NI SHILINGI **10,000** TU.
7. FANYA HARAKA KUJISAJILI, NAFASI NI CHACHE.